

SABATO

Papa Gregory XIII Alipobadilisha Kalenda: Siku Zilivurugwa, Sabato Ilipotea?

Mamilioni ya watu leo hii, wanashikilia ufahamu kwamba ni vigumu sana kujua hasa kwamba siku ya Jumamosi ni lini kwa sababu wakati flani katika kalenda, kuna siku zilipotea...

MCH. ALMODAD AMOS YARAGWILLER

2026

Utangulizi

Mamilioni ya watu leo hii, wanashikilia ufahamu kwamba ni vigumu sana kujua hasa kwamba siku ya Jumamosi ni lini kwa sababu wakati flani katika kalenda, kuna siku zilipotea kutokana na tukio la kurekebishwa kwa kalenda. Je, jambo hili linaukweli kiasi gani ndani yake? Na Je, ikiwa ni kweli kalenda ilibadilishwa tunaweza kuitambua tena siku ya Sabato?

Je, tunaweza kujua kwa uhakika kwamba Jumamosi tunayoijua leo ni ile ile Jumamosi waliyoijua Musa na Yesu? Jibu ni rahisi kabisa na dhahiri, Ndio! Na katika hili tunao ushahidi mwingi sana na wa kutosha kabisa.

Je, Mungu Angenyaza tu Wakati Sabato Inapotea?

Kwanza kabisa, ni ushahidi wa Jamii ya Wayahudi ambao wamekuwa wakiishika siku ya saba tangu wakati wa baba yao, Ibrahimu, na bado wanaendelea kuishika hata sasa. Hawajawahi kuipoteza katika zama zote za Histori. Huenda mahali ambapoingekuwa rahisi kabisa kuipoteza na hatimaye kuvurugika kwa siku hii ilipaswa iwe wakati Israeli wao jangwani. Lakini hata hapo Mungu alikuwa na mpango wa kuihifadhi salama kabisa. Sura ya 16 ya Kutoka inasimulia mfululizo wa miujiza ya Sabato ya kila wiki iliyorudiwa kwa muda wa miaka 40 wakati Wayahudi walipokuwa wakizunguka-zunguka jangwani. Kwa mfano, Mungu aliwapa wana wa Israeli mana waikusanye kwa siku sita kwa wiki, lakini Bwana aliwaamuru wakusanye mara mbili zaidi siku ya Ijumaa kwa sababu hakuna mana ambayo ingeanguka kutoka mbinguni siku ya Sabato. (Kumbuka, hii ilikuwa kabla ya kuwapa Amri Kumi.) Mungu alisisitiza tena juu ya suala la utunzaji wa Sabato huko Sinai (Kutoka 20:8-11)

wakati alipowapatia sheria; na haikuishia hapo, Wayahudi walikuwa bado wanaishika siku ya saba kama siku ya Sabato mpaka wakati Yesu alipozaliwa. Taifa zima la Israeli limekuwa likihesabu kwa uangalifu mkubwa na kuuzingatia wakati, wiki baada ya wiki, kwa maelfu ya miaka. Labda tuseme, mtu mmoja, yaani Myahudi mmoja ambaye labda alifungwa gerezani anaweza kupoteza hesabu na sikumbuke kwamba Siku ya Sabato ni lini hasa, lakini ni jambo ambalo haliwezekani katu-katu kwa taifa zima na Wayahudi wote kusahau au kukosea hesabu ya siku yao takatifu, ambayo wameendelea kuiheshimu kwa miaka na miaka. Tafakari jambo hili.

Namba Mbili, zaidi ya lugha 160—za kale na za kisasa—duniani kote zinaitambua siku ya Jumamosi kama “siku ya mapumziko.” Kwa mfano, neno la Kihispania la Jumamosi ni “Sábado,” linalomaanisha Sabato. Warusi wanaiita “Subbota.” Inaonekana wazi kwamba wakati lugha hizi za kale zilipozaliwa, Jumamosi ilikuwa ikitambuliwa ulimwenguni kote kama siku ya mapumziko na iliingizwa katika jina lenyewe la siku hiyo.

Tatu, Mungu ameahidi kuihifadhi Sabato milele na milele. Isaya 66:22,23 inasema, “ ‘Kwa maana kama mbingu mpya na nchi mpya nitakazofanya zitakavyokaa mbele zangu,’ asema Bwana, ‘ndivyo wazao wenu na jina lenu watakavyokaa. Na itakuwa, mwezi mpya hata mwezi mpya, Sabato hata Sabato, wanadamu wote wenye mwili watakuja kuniabudu mbele zangu,’ asema Bwana.” Je, hivi kweli kabisa Mungu angepoteza hesabu ya siku, na kuipoteza Sabato ikiwa ameahidi kwamba itashikwa milele na milele? Hii nayo inahitaji kutafakati tena.

Ushahidi wa Nne, Kulingana na Agano Jipya, Yesu alikufa siku ya Ijumaa na akafufuka siku ya Jumapili, siku ya kwanza ya juma. Biblia inasema “akaja mtu, jina lake Yusufu, mtu mwenye heshima, naye alikuwa akingojea ufalme wa Mungu. Huyu alikwenda kwa Pilato, akaomba mwili

wa Yesu. Akautoa, akaufunga kwa sanda, akauweka katika kaburi lililochimbwa mwambani, ambalo ndani yake hawakuwa wamemweka mtu bado. Siku hiyo ilikuwa siku ya Maandalio, na Sabato ilikuwa karibu kuanza" (Luka 23:52-54). Ijumaa iliitwa "siku ya maandalio" kwa sababu ilikuwa wakati wa kujiandaa kwa Sabato.

Mistari michache inayofuata inasema, "Wanawake waliokuwa wamefuatana naye kutoka Galilaya walifuatana naye, wakaliangalia kaburi, na jinsi mwili wake ulivyowekwa. Kisha wakarudi, wakaandaa manukato na marhamu. Wakapumzika siku ya Sabato, kama ilivyoamriwa" (f. 55, 56). Huu ni wakati mzuri wa kukumbuka kwamba wafuasi wa Yesu hawakuweza hata kumaliza kazi yao ya upendo, ya kuupaka manukato mwili wa Bwana wao kwa ajili ya mazishi, mpaka Sabato ilipopita. Ina maana kwamba lazima waliamini Yesu aliikumbuka sana na kuitunza amri ya Kuikumbuka siku ya Sabato na kuitakasa.

Angalia pia kwamba wanawake hawa walipumzika siku ya Sabato "kama ilivyoamriwa"—maana yake amri ya nne—inayosema, "Siku ya saba ni Sabato," kwa hiyo tunaweza kujua walikuwa wakipumzika siku ya Jumamosi. Mistari inayofuata mara moja inasema, "Hata siku ya kwanza ya juma, alfajiri na mapema, walikwenda kaburini, wakiyaleta manukato waliyoyaandaa. Wakalikuta jiwe limevingirishwa mbali na kaburi" (Luka 24:1, 2). Biblia Toleo la Habari Njema inasema: Jumapili, alfajiri na mapema. Hakika si vigumu kuitambua siku saba ya Juma, na hivyo si vigumu kujua kwamba ni siku gani hasa inapaswa kuwa siku ya Sabato. Ukiisha kujua kwamba Jumapili ndiyo siku ya kwanza ya Juma, utajua pia kuwa Jumamosi ndiyo siku ya Sabato.

Kulingana na Biblia, Yesu alikufa Ijumaa, siku ya maandalio, ambayo Wakristo wengi leo hii huiita "Ijumaa Kuu." Kisha "alipumzika" kaburini siku ya saba, yaani siku ya Sabato, ambayo ni siku ya Jumamosi. Kisha

siku ya Jumapili, siku ya kwanza ya juma, Yesu alifufuka kutoka kaburini. Kwa kweli inashangaza unapotafakari kwamba Yesu aliishika Sabato hata katika kifo chake. Alikamilisha kazi yake ya wokovu Ijumaa mchana —akitangaza, “Imekwisha!”—kisha akafa. Alipumzika kaburini katika Sabato yote na kisha akafufuka Jumapili asubuhi. Kwa nini? Kuendelea na kazi yake, sasa akiwa kuhani mkuu wetu (Waebrania 8:1-3).

Uhusiano wa Mabadiliko ya Kalenda na Utunzaji wa Sabato

Mwaka 1582 ni mwaka wenye tukio kubwa kabisa la kihistoria ambalo ni muhimu kulifahamu ili kuweza kujibu swali lililoko mezani. Ni kweli kabisa kwamba mnamo mwaka 1582, Papa Gregory XIII alifanya mabadiliko madogo kwenye kalenda, lakini mabadiliko aliyoyafanya hayakuhusiana wala hayakuingilia mzunguko wa seti ya siku saba za wiki.

Kalenda tunayoitumia leo hii inaitwa Kalenda ya Gregory na iliitwa kwa jina lake wakati alipoidhinisha mabadiliko haya. Kabla ya 1582, kalenda iliyokuwa ikitumika ilikuwa kalenda iliyoitwa Kalenda ya Julian. Kalenda hii ilianzishwa Kaisari Julius yapata mwaka 46 KK.

Lakini kalenda ya Julian ilikuwa na kawaida ya kuuhesabu mwaka kuwa una-urefu siku 365 na 1/4, lakini ukweli ni kwamba kwa kawaida, mwaka ukihesabiwa kulingana na mzunguko wa jua, unakuwa mfupi kwa dakika 11 kuliko ulivyo mwaka katika Kalenda ya Julian. Sasa, hizi dakika 11zilikuwa zikiendelea kujikusanya na kujikusanya kila mwaka, kiasi kwamba ilipofika mwaka 1582, hizo dakika kumi kwa kila mwaka zilikuwa zimefikisha jumla ya siku 10 kamili kwa kuzingatia mfumo wa mzunguko wa Jua. Papa Gregory aliondoa tu siku hizi kumi kutoka kwenye kalenda.

Tukio hili lilifanyika siku ya Alhamisi, Oktoba 4, 1582, na siku ya Ijumaa ambayo ni siku iliyokuwa inafuata ilipaswa iwe Oktoba 5, lakini Gregory aliifanya kuwa Oktoba 15 badala yake, akiondoa siku 10 ili kuirudisha kalenda katika uwiano mzuri ulioendana na mzunguko wa jua, ambao hasa ndio kipimo cha majira na nyakati.

Siku za juma hazikubadilishwa. Ijumaa bado ilifuata baada ya siku ya Alhamisi, na Jumamosi bado ilifuata baada ya siku ya Ijumaa. Siku ya saba ilibaki Jumamosi, kama ilivyokuwa daima. Hata mashirika makubwa kabisa ulimwenguni yanayojishughulisha na kuweka kumbukumbu za nyakati na majira yanathibitisha ukweli huu:

> “Hakujakuwa na mabadiliko yoyote katika kalenda yetu katika karne zilizopita ambayo yameathiri kwa njia yoyote mzunguko wa wiki.” — James Robertson, Mkurugenzi American Ephemeris, Idara ya Jeshi la Maji, U.S. Naval Observatory, Washington, D.C.

> “Inaweza kusemwa kwa uhakika kwamba hakuna siku iliyopotea tangu Uumbaji, licha ya mabadiliko yote ya kalenda, hakujawa na kukatika kwa mzunguko wa wiki.” —Dkt. Frank Jeffries, Mwanachama wa Jumuiya ya Kifalme ya Astronomia na Mkurugenzi wa Utafiti wa Royal Observatory, Greenwich, England.

Hitimisho

Katika safari hii ya muda, tangu enzi za manabii hadi wakati wetu huu, Jumamosi imesimama imara kama nguzo isiyoyumba. Ushuhuda wa taifa la Israeli, lugha nyingi za dunia, na ahadi thabiti ya Mungu mwenyewe zinatuhakikishia kwamba siku hii tunayoijua kama Jumamosi

ni ile ile siku takatifu ambayo Mababa wa Imani waliishika kwa ibada na heshima. Hata katika kifo chake, Bwana wetu Yesu Kristo aliitunza Sabato, akitufundisha umuhimu wake usiofifia. Licha ya mabadiliko ya kalenda na kupita kwa takribani karne na karne, mzunguko wa wiki umebaki kuwa ushuhuda wa uaminifu wa Mungu na mpango wake kwa ajili ya pumziko la wanadamu. Kwa hivyo, tunapoiingia kila Jumamosi, na tujue kwa uhakika kwamba tunaingia katika siku iliyobarikiwa na kuwekwa wakfu tangu mwanzo, siku ambayo inatuunganisha na historia ya imani na inatuandaa kwa ajili ya pumziko la milele katika uwepo wake. Jumamosi bado ni Jumamosi, zawadi kutoka kwa Muumba wetu, inayoendelea kutukumbusha upendo wake usio na mwisho.

ISAYA 66:22,23

> 'Kama vile mbingu mpya na nchi mpya, nitakazofanya, zitakavyokaa mbele zangu, asema BWANA, ndivyo uzao wenu na jina lenu litakavyokaa. 23 Na itakuwa, mwezi mpya hata mwezi mpya, na sabato hata sabato, wanadamu wote watakuja kuabudu mbele zangu, asema BWANA.'

Source: Sehemu kubwa ya makala hii imechukuliwa katika gazeti la **The Rest of Your Life**. lililotolewa na The Amazing Facts Inc. kwa makusudi ya kutoa elimu ya yote unayohitaji kufahamu kuihusu sabato, ili kupata Gazeti zima na elimu zaidi kuhusu Sabato bofya hapa au tembelea tovuti iliyosheheni yote yanayoihusu Sabato, tangu edeni mpaka habari za hivi karibuni kuihusu Sabato. Ni katika tovuti inayoitwa **Sabbath Truth**.



Pakua Kitabu hiki kidogo kinachofafanua zaidi juu ya Fundisho la Biblia kuhusu kwa nini Mungu hakumuua Shetani mara uovu ulipotokea? na Kwa nini kuna uovu duniani wakati Mungu ni mwema kabisa? Kitabu hiki kimeandikwa na Mchungaji Almodad Amos Yaragwiller. Pakua sasa PDF ...

Soma na upakue “Pambano Kuu” (PDF) →

Zaidi kutoka Injili Milele

Makala, vitabu, video na sauti zaidi zinapatikana kwenye maktaba ya Injili Milele:

Je, Sabato Ilikoma kwa Kuwa Ilikuwa Kivuli cha Mambo Yajayo?
Sabato · PDF

Sanduku la Agano: Je, Litaonekana Tena?
Unabii · PDF

Nini Hasa Maana ya Kibiblia ya Maneno ya Baba: “Mimi Leo Nimekuzaa”?
Uungu · Video

Je, Yesu ni “Mungu Mwana” au “Mwana wa Mungu”?
Uungu · Video

Kwa Nini Mungu Alimuumba Lusifa?
Pambano Kuu · PDF

Je, ni Lazima Kupiga Magoti Wakati wa Maombi?
Ibada · PDF

Injili Milele

almodad-2.github.io/injili-milele/sw/

WhatsApp +255 718 834 621 · modaofhope@gmail.com

© 2026 Pr. Almodad Amos Yaragwiller · Injili Milele. Haki zote zimehifadhiwa. Usiuze nakala hii bila ruhusa ya maandishi ya mwandishi.